

FURSA ZA UTALII NA UWEKEZAJI

SHUGHULI ZA UTALII:

- Kuogelea na kupiga mbizi na kuzamia (snorkeling and diving).
- Kutazama nyangumi, kasa wa baharini na viumbe wengine wa baharini
- Kutembelea magofu ya kale ndani ya Hifadhi
- Kutalii kwa kutumia boti ya kioo (Glass-bottomed Boat)
- Kuweka kambi za usiku kisiwani (Night Camping)
- Kufurahia vyakula vya baharini Kisiwani
- Ziara za kielimu na utafiti

FURSA ZA UWEKEZAJI:

- Kuwekeza katika Ujenzi wa miundombinu ya utalii endelevu kama vile hoteli, migahawa
- Uwekezaji katika kambi za usiku (Night Camping Sites)
- Uwekezaji katika Usafiri wa Majini kwa ajili ya Utalii
- Uwekezaji katika michezo ya baharini
- Ushirikiano katika miradi ya uhifadhi na elimu ya mazingira.



MAWASILIANO

S.L.P 7565, Upanga, Mtaa wa Olympio, Dar es Salaam, Tanzania

+255 (0) 22 2150 621

marineparks@marineparks.go.tz

www.marineparks.go.tz

marineparkstz



WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU (MPRU)



TUNAHIFADHI BAHARI KWA MAENDELEO ENDELEVU

LINDA
BAHARI

HIFADHI
RASILIMALI

JENGA
MAENDELEO

FAIDIKA
KIUCHUMI

HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU TANZANIA (MPRU)

Ni kitengo kilichoanzishwa chini ya sheria Na.29 ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu ya Mwaka 1994 na kupewa jukumu la Kuanzisha, kusimamia na kuendeleza rasilimali za bahari ikiwemo viumbe na mazingira ya bahari kwa matumizi endelevu ya bahari Tanzania.

KAZI ZA MPRU

- Kuanzisha,kusimamia na kuendeleza matumizi endelevu ya rasilimali za Bahari Tanzania
- Kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa bahari.

MPRU INAHIFADHI NINI?

Inahifadhi rasilimali za bahari kama vile Matumbawe, samaki, wanyama wa bahari, nyasi za bahari, fukwe,mikoko.



KWA NINI TUNAHIFADHI?

- Kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za bahari.
- Kulinda bayoanuwai na mazingira ya asili.
- Kusaidia maendeleo ya kiuchumi kupitia utalii na uvuvi endelevu.

FAIDA ZA UHIFADHI

- Kuongezeka kwa samaki na viumbe wa baharini.
- Fursa za ajira kupitia utalii na utafiti
- Ziara za kielimu na utafiti.

JUKUMU LA JAMII KATIKA UHIFADHI :

- Kushiriki katika shughuli za uhifadhi na ufuatiliaji.
- Kutoa taarifa kuhusu uharibifu wa mazingira.
- Kuelimisha wengine kuhusu umuhimu wa kuhifadhi bahari.

FAIDA ZA UHIFADHI KWA JAMII

- Kuongezeka kwa kipato kupitia utalii ,uvuvi, kilimo cha mwani,ufulaji majongoo bahari.
- Upatikanaji wa mafunzo na ujuzi mpya kutoka katika miradi mbali mbali inayosimamiwa na MPRU ,Mashirika na Wadau wa Uhifadhi nchini.
- Kuboresha maisha kupitia mazingira safi na salama.

MAMBO YA KUFANYA NA KUEPUKA NDANI YA HIFADHI:

MAMBO YA KUFANYA:

- Kuheshimu mipaka ya hifadhi.
- Kuripoti shughuli zisizozingatia sheria
- Kushiriki katika shughuli za uhifadhi.
- Kuwezesha shughuli za utafiti na utalii endelevu.

MAMBO YA KUEPUKA :

- Uvuvi usiozingatia sheria na matumizi ya vilipuzi.
- Kukata mikoko na kufanya shughuli za kiuchumi katika Hifadhi bila kibali.
- Kutupa taka baharini

ADHABU:

- Faini au kifungo kwa ukiukaji wa sheria na kanuni za uhifadhi.

